

Ninaweza Kurudi Kazini Lini ikiwa Mtu Ninayeishi Naye ana Ugonjwa wa COVID-19? Nakala

Mtu ninayeishi naye ana ugonjwa wa COVID-19. Ninaweza kurudi kazini lini? Ikiwa mtu unayeishi naye ana ugonjwa wa COVID-19, kaa nyumbani kisha ufuate miongozo hii hata kama unajihisi mwenye afya au tayari kipimo kinaonyesha huna COVID-19.

Mjulisha msimamizi wako kisha ufanyie nyumbani ikiwa una uwezo. Ikiwa unafanya kazi katika miundombinu muhimu na kutokuwepo kwako kunaweza kuleta upungufu wa wafanyakazi, unaweza kwenda kufanya kazi lakini uvae maski na ukae mbali na wafanyakazi-wenza na wageni umbali wa futi 6 (mita 2).

Ukiwa nyumbani, jitenge mbali na jamaa wako aliye mgonjwa, na usishiriki chochote na mtu kama vyombo au simu kwa siku 14. Baada ya siku 14, unaweza kurudi kazini kama kawaida.

Endelea kujitenga mbali na jamaa wako aliye mgonjwa hadi ajihisi salama na hadi vitu hivi vifanyike:

1. Dalili zao, kama kikohozi au kupungukiwa na pumzi ziboreke.
2. Imekuwa angalau siku 10 tangu dalili zao zianze.
3. Wamekuwa na saa 24 bila kuwa na homa ya joto na bila dawa ya kupunguza joto ya homa.

Ikiwa huwezi kujitenga na jamaa wako aliye mgonjwa nyumbani kwenu. Ongea na daktari wako, kliniki au mtu wa afya ya umma unayeweza kuwasiliana naye ili mjadiliane ni kwa muda gani unapaswa kukaa nyumbani. Kwa ujumla, unapaswa kukaa nyumbani hadi mtu wa familia aliye mgonjwa ajihisi salama na tena siku 14 za ziada.

Ikiwa utapata dalili za ugonjwa wa COVID-19, ongea na daktari wako au kliniki ya eneo lako kuhusu kupimwa. Kama ilivyo na jamaa wako aliye mgonjwa, kaa nyumbani hadi dalili zako ziboreke, imekuwa angalau siku 10 tangu dalili zako zianze, na umekuwa na saa 24 bila homa ya joto na bila dawa ya kupunguza homa ya joto.

Kwa taarifa zinazochipuka kuhusu COVID-19 tembelea health.mn.gov

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

08/10/20

When Can I Return to Work if Someone Living With Me is Sick With COVID-19? (Swahili)

To obtain this information in a different format, call: 651-201-4989